SERA G015: SERA YA KUPAMBANA NA ULAGHAI NA RUSHWA

Mtu mwenye wajibu:	CEO	Toleo:	1.1
Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi leo:	27 February 2019	Tarehe ya marekebisho yaliyopangwa:	Februari 2021

UTANGULIZI

Sera hii iliandikwa na Ofisi ya So They Can ya Australia ili itumike katika shughuli zote za So They Can.

So They Can inaendesha taasisi tano ambazo zimesajiliwa nchini Australia, New Zeland, Marekani, Kenya na Tanzania.

So They Can Australia ni ofisi ya kimataifa inayotoa usaidizi kwa taasisi zote za So They Can. Wakati wote Mkurugenzi Mtendaji ina maana ya Mkurugenzi Mtendaji wa So They Can Australia, Kenya na Tanzania. Isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo, Bodi ina maana ya Bodi husika ya taasisi ya So They Can ambapo umeajiriwa au ulipopangiwa.

UFAFANUZI

Ulaghai

Sera hii inatumia neno ulaghai kama ilivyofafanuliwa wa Mfumo wa Udhibiti wa Udanganyifu wa “Commonwealth” wa 2014 kama ' kujinufaisha kwa njia ya udanganyifu au kusababisha hasara kwa kudanganya au njia nyingine'. Hii ni pamoja na:

- Wizi
- Kujipatia mali, faida ya kifedha au faida nyingine yoyote kwa udanganyifu
- kusababisha hasara, au kuepuka au kutengeneza dhima kwa udanganyifu
- Kutoa taarifa za uwongo au za kupotosha, au kushindwa kutoa taarifa pale ambapo kuna wajibu wa kufanya hivyo
- kutengeneza, kutumia au kuwa na nyaraka zilizoghushiwa
- rushwa au matumizi mabaya ya nafasi
- Matumizi kinyume cha sheria ya kompyuta, magari, simu na mali nyingine au huduma
- kutoa taarifa za siri kwa vyanzo vya nje
- kuingilia mfumo wa kompyuta, na
- Makosa mengine yoyote yanayofanana na yaliyoorodheshwa hapo juu.

Kwa sababu ya hatari iliyoongezeka ya kuendesha programu katika mazingira magumu ya nje ya nchi na kwa kuzingatia Mwongozo wa Ulaghai na udanganyifu na kupambana na rushwa kwa

washirika wa DFAT, So They Can imeongeza ufafanuzi huu kwa kuzuia wazi kabisa malipo yote ya uwezeshaji.

Malipo ya uwezeshaji yamefafaanuliwa chini ya kifungu cha 70.4 cha Sheria ya makosa ya Jinai ya Australia ya 1995. Kanuni hii inafafanua kwamba haya ni malipo kwa viongozi wa umma wa kigeni kwa lengo la pekee au kubwa la kuharakisha au kupata huduma za kiserikali za kawaida. Malipo ya uwezeshaji hayana tofauti na rushwa katika nchi nyingi.

Rushwa – Kwa So They Can rushwa inamaanisha matumizi mabaya ya madaraka ili kujinufaisha. Rushwa inaweza kuwa kubwa au ndogo, yenye asili ya kisiasa na kwa kawaida hufanyika kwa lengo la faida ya kifedha.

- Rushwa kubwa inaweza kuhusisha vitendo vinavyopotosha sera au utendaji wa jumla wa Serikali.
- Rushwa ndogo ndogo inahusu matumizi mabaya madaraka ya viongozi wa serikali wa ngazi ya chini.
- rushwa ya kisiasa ina maanisha matumizi mabaya ya madaraka kupotosha sera za taasisi kwa faida ya kisiasa.

Wawakilishi wa So They Can - ni watu wote na taasisi zote zinazofanya kazi kwa niaba ya So They Can bila kujali kama kuna au hakuna makubaliano rasmi ya kisheria kati yao na na So They Can. Hii inajumuisha, mbali na wenginge, wadhamini wote, wanachama, wakurugenzi, wafanyakazi, wakandarasi, washauri, wafanyakazi wa kujitolea, na washirika wanaotekeleza miradi bila kujali ni nchi gani majukumu yao yamepangwa. Katika waraka huu So They Can ina maana ya taasisi yoyote au taasisi zote za kimataifa za So They Can zilizosajiliwa nchini Australia, New Zealand, Kenya, Tanzania na Marekani.

TAMKO LA SERA

So They Can ina wajibu kwa wadau wote kuhakikisha kuwa rasilimali zote za kifedha na hali na mali zinazotumiwa na zinazotolewa na So They Can zinatumika tu kwa madhumuni yaliyoelezwa na kwamba taratibu zinawekwa ili kulinda fedha hizo dhidi ya udanganyifu huko Australia lakini na katika nchi nyingine zote ambako So They Can inafanyakazi.

So They Can itafuata sheria zote zinazohusika na kukabiliana na rushwa na shughuli za udanganyifu katika mamlaka zote ambako inafanya kazi na inategemea washirika wote wa mradi kutekeleza sheria husika katika mamlaka zao.

Wawakilishi wote wa So They Can wanapaswa kutoa ripoti bila kuchelewa kuhusu majaribio yote ya utendandaji kosa la ulaghai, tuhuma au udanganyifu uliobainika. Matukio yote ya

udanganyifu na rushwa yanashughulikiwa kwa njia ya siri, kwa wakati na kitaalamu kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sera ya Malamiko na Sera ya Kutoa taarifa za So They Can.
Ulaghai au rushwa yoyote iliyothibitishwa itakuwa ni sababu ya kufukuzwa kazi. Matukio makubwa ya udanganyifu, iwe ni tuhuma au imethibitika, yataripotiwa kwenye vyombo husika vyenye mamlaka.

KANUNI

Sera ya Ulaghai na Kupambana na Rushwa ya So They Can imejikita kwenye kanuni za "kutokuvumilia kabisa" ambazo katika utekelezaji inamaanisha kwamba So They Can itafanya yafuatayo:

- kuchunguza matukio yote au madai ya udanganyifu na rushwa ili kuamua hali na kiwango cha udanganyifu
- kutumia vikwazo sahihi vya utawala au mikataba, ikiwa ni pamoja na kusitisaha mkataba
- kuwaripoti wahalifu ili washitakiwe na matumizi ya adhabu zinazofaa, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha kwenye mamlaka za kutekeleza sheria za nje ya nchi na / au Shirikisho la Polisi la Australia, na
- kufuatilia urejeshwaji wa fedha na mali zilizoibiwa

Mkakati wa kutokuvumilia kabisa ulaghai na rushwa haumaanishi kwamba udanganyifu wote na rushwa zinaweza kuepukwa au kuzuiwa. Badala yake mbinu ya kutokuvumilia kabisa inawakilisha kanuni na mbinu ambazo hutumiwa na So They Can kuzuia, kutambua, kuchunguza na kufuatilia udanganyifu na rushwa ili kudhibiti kwa ufanisi hatari zilizopo.

UTEKELEZAJI WA SERA

Kwa kupitisha Sera hii Menejimenti ya So They Can ina nia kufanya yafuatayo:

- Kupitisha njia ya usimamizi wa kuzuia hatari, kutambua na uchunguzi wa shughuli za udanganyifu zilizosababishwa ambazo zinaingizwa katika mchakato wake wa shughuli, shughuli za usimamizi, udhibiti wa ndani na shughuli zinazohusiana;
- Mafunzo kwa wawakilishi wa So They Can juu ya maadili, faragha na udanganyifu na uelewa wa rushwa ikiwa ni pamoja na wajibu wao wa kutoa taarifa za udanganyifu ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kubainika.
- Kusaidia michakato ya ndani na ya nje ya utoaji taarifa salama juu ya uovu (Sera ya Kutoa taarifa Sera ya Malamiko za So They Can na kuhakikisha kwamba wawakilishi wa So They Can wamepata mafunzo juu ya sera hizi na wanafahamu taratibu za kutoa taarifa na uchunguzi.
- Kuwashitaki na matumizi ya adhabu sahihi dhidi ya wale ambao wamefanya udanganyifu.

- Kuzingatia Sera ya Mwingiliano wa Maslahi ya So They Can ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Wawakilishi wa So They Can hawafanyi au hawasaidii kufanyika, kupokea au kutafuta kupokea ofa yoyote, zawadi, malipo au faida ya aina yoyote, ambayo yanaweza kuwa haramu au kitendo cha rushwa.
- Kuripoti kesi za udanganyifu zinazodhaniwa kutendwa kwa wafadhili na kuchukua hatua zote muhimu ili kurejesha fedha na mali zilizoibiwa. Kuwajulisha wafadhili mara kwa mara juu ya maendeleo ya jitihada za urejeshwaji fedha na mali zilizoibiwa kutokana na ulaghai au rushwa.
- Kusimamia fedha na mali za programu ikiwa ni pamoja na matumizi ya madaftari kumbukumbu ya mali.

RELATED DOCUMENTS

- So They Can Policy and Manual Register
- So They Can Whistleblowing Policy
- So They Can Complaints Policy
- So They Can Conflict of Interest Policy
- So They Can Finance Manual
- DFAT Fraud & Anti-corruption Guidance for DFAT Partners